

Muhtasari wa Mafunzo ya Mbali kwa Familia

Daraja za K hadi 4

Yaliyomo	Maoni ya Muda
Masomo ya Kusoma na Kuandika (Tazama somo fupi, na/au Kamilisha funzo la mtandao)	Dakika 10-20 kila siku
Kusoma (Soma vitabu, tazama vitabu zikisomwa kwa sauti ya juu, Sikiliza kitabu)	Angalau dakika 20 kila siku (Inaweza kuhusu sayansi, masomo ya jamii, n.k)
Kuandika au Shughuli ya Neno au Sauti ya Maneno/Msamiati	Dakika 20-30 kila siku
Hesabu	Dakika 30 kila siku
Sayansi	Dakika 45 kila wiki
Masomo ya Jamii	Dakika 30 kila wiki
Sanaa, Elimu ya Kimwili, au Elimu ya Kijamii na Kihisia	Dakika 30 kila siku

Kila wiki, Mpango wa Mafunzo ya Mbali utakuwa na yafuatayo:

Mafunzo ya mbali kwa wanafunzi wa shule ya msingi utaangazia katika mada ya masomo. Sanaa za Lugha ya Kiingereza na Hesabu hufaa kufanyika kila siku, pamoja na shughuli za kimwili, machunguzi ya sanaa, **au** kuangazia juu ya ustawi (Mafunzo ya Kijamii na Kihisia). Maoni ya Sayansi na Masomo ya Jamii ni kila wiki, kwa hivyo familia wataamua wakati gani unafaa zaidi kulingana na ratiba yao, iwapo yote kwa mara moja, au kiasi kidogo kila siku. Mpango uliyoainishwa hapa chini una mada zote za masomo.

❖ Mafunzo ya Mbali:

- Mwalimu wa mtoto wako atawasiliana nawe ili kupanga wakati wa kufuatilia wanafunzi na kujadiliana kuhusu chaguo za kusaidia mwanafunzi kwa mafunzo ya mbali . Baadhi ya chaguo hizo zinaweza kuwa barua pepe, kuwasiliana kutumia Google Classroom, DOJO, Remind, au jukwaa zinginezo, au kuwa na vipindi vya kufuatilia wanafunzi kutumia Zoom au Google Hangouts. Mbinu hizi zitabadilika kulingana na darasa, na shule. Shule yako itawasiliana na familia moja kwa moja ili kutoa habari hii.

❖ Kazi za Nyumbani za Kila Wiki:

- Kila wiki wanafunzi watapokea shughuli zinazolingana na mpango wa mafunzo ya mbali. Hizi zitabadilika kutoka mada moja hadi nyingine na zinafaa kufanyika kwa sehemu nyingi na wanafunzi pekee yao. Wanafunzi wetu wachanga zaidi kwa uwezekano mkubwa watahitaji usaidizi katika kusoma mara nyingi. Miradi zinaweza kuwa na kusoma na kuandika kuhusu kitabu kinachopendwa na mwanafunzi, au kufanya hesabu, au kuchunguza mawazo ya sayansi na masomo ya jamii.
- Wanafunzi wataulizwa kuwasilisha kazi kutoka shughuli kadhaa. Matarajio ya kazi yataelezewa na maagizo kutoka mwalimu wao.
- Iwapo wanafunzi watahitaji usaidizi au ufafanuzi zaidi kuhusu shughuli waliyopatiwa, wanaweza kumtumia mwalimu barua pepe au kuomba usaidizi kutumia mbinu ya mawasiliano iliyochaguliwa na mwalimu wa mwanafunzi.
- Kwa wanafunzi wanaopokea huduma za elimu maalum, shughuli zitabadilishwa zinavyofaa kutumia ushirikiano kati ya mwalimu wa darasa na mwalimu wa elimu maalum.
- Mtoto wako pia anaweza kupendekezewa fursa za kujifunza kutumia mtandao kama iReady, Lexia, Raz Kids, ST Math, au Khan Academy.
- Kazi za nyumbani ni za hiari, lakini tunamtia moyo mtoto wako kuzikamilisha.

❖ Mikutano ya Mtandao na Wanafunzi:

- Ndani ya wiki mzima kutakua na muda fulani ambazo walimu wataweza kupatiikana kwa mikutano ya mtandao. Hapa ndipo mawasiliano ya mwalimu/mwanafunzi yanaweza kukuzwa na usaidizi wa kibinafsi unaweza kupatikana, unavyohitajika.
- Wakati wa mikutano ya mtandao yataratibishwa kwa namna inavyoweza chaguo ya asubuhi au jioni kila siku wiki mzima ili kupatia nafasi ratiba ya wanafunzi wengi iwezekanavyo.
- Walimu watawasiliana nawe kuhusu maelezo ya mikutano haya ya mtandao.
- Kushiriki katika mikutano haya ni hiari kwa wanafunzi.
- Kwa wanafunzi wanaopokea huduma za elimu maalum ya kutolewa kwa darasa la kawaida, watoa huduma wa elimu maalum watakuwa na muda tofauti ili kuwasiliana na wanafunzi ambao wanapokea huduma, inavyofaa.
- **Tafadhali hakikisha umefanya mapitio ya tabia inavyofaa na mtoto wako kabla ya mikutano haya ya mtandao.**

❖ Kuwasilisha Kazi:

- Wanafunzi watawasilisha kazi katika wakati unaofaa uliyopangwa na walimu wa mwanafunzi.
- Kazi inafaa kuwasilishwa kwa walimu kutumia mbinu inayopendekezwa na mwalimu.
- Mabadiliko muhimu au kupewa nafasi zaidi kwa wanafunzi wanaopokea huduma za elimu maalum ili kuwasilisha kazi (kwa mfano kuongezewa muda, n.k) yatawasilishwa.

❖ Taarifa Zaidi:

- Unaweza kuendelea kutumia mipango ya “Kujifunza Nyumbai” yaliyoandaliwa kwa Wiki ya 1-4 katika Tovuti ya LPS Kujifunza Nyumbani. Rasilimali zaidi zitaendelewa kuongezewa kwa ukurasa huu.
- Tunawatia moyo familia kuandaa ratiba zao wenyewe unaolingana na hali yao ya kipekee. Tunakutia moyo kupitia maagizo ya kujifunza kwa mbali, shughuli zilizoambatana nazo alizopewa mwanafunzi, na fursa za muda wa mkutano wa mtandao utakazopokea wiki hii. Halafu, ukiwa na mtoto wako, panga ratiba ya wiki hiyo inayolingana na familia yako.
- Watoto wengi hupata matokeo bora zaidi wakati kuna matarajio na ratiba yanayoweza kutabiriwa. Labda unaweza kutumia wiki hii huku ukifafanua maeneo ya shughuli, kuweka matarajio wazi wa mbinu ya kukamilisha kazi inayotakikana kwenda mbele (*kwa mfano*, kariri kuingia katika akaunti, kutayarisha vifaa vya masomo karibu na kompyuta na/au meza ya kazi, kuweka saa ili kuwezesha kufanya kazi kwa muda fulani unaofaa)